



# Ripoti Ya Uwajibikaji

Ufanisi, Rushwa na Ubahirifu  
Katika Sekta ya Umma  
2021

**MAPATO YA SERIKALI**

**BENKI**

**NYUMBANI**







# Ripoti Ya Uwajibikaji

## Ufanisi, Rushwa na Ubahirifu Katika Sekta ya Umma 2021



Co-funded by European Union





# YALIYOMO

<b>UTANGULIZI .....</b>	<b>ii</b>
<b>SEHEMU YA KWANZA .....</b>	<b>1</b>
<b>MAANA YA UKAGUZI WA UFANISI NA VIASHIRIA VYA RUSHWA, UDANGANYIFU NA UBADHIRIFU ...</b>	<b>1</b>
Maana ya Ukaguzi wa Ufanisi .....	1
Maana ya Viashiria vya rushwa, udanganyifu na ubahirifupi: .....	1
Vigezo Viliviyotumika Kubainisha Viashiria vya Rushwa, Udanganyifu na Ubahirifupi .....	1
<b>SEHEMU YA PILI .....</b>	<b>3</b>
<b>UCHAMBUZI WA RIPOTI ZA UKAGUZI WA UFANISI.....</b>	<b>3</b>
Jambo la 1: Mapungufu Kwenye Ufuatiliaji wa Miradi Iliyotekelizwa Kwa Utaratibu wa “Force Account” Katika Sekta Ya Elimu .....	3
Jambo la 2: Udhafu katika Mifumo ya TEHAMA.....	5
Jambo la 3: Utolewaji wa Vitambulisho vya Taifa Usioridhisha .....	8
Jambo la 4: Uchakavu na Uchafu katika Masoko ya Chakula .....	10
Jambo la 5: Mapungufu katika Ukusanyaji wa Kodi ya “Uhamishaji Gharama” ya Mauziano .....	13
Jambo la 6: Utekelezaji Usioridhisha wa Mradi wa Uzalishaji wa Sukari Mbigiri.....	14
Jambo la 7: Utekelezaji wa Mapendekezo Yaliyotolewa Katika Baadhi ya Kaguzi Za Ufanisi za mwaka 2016 .....	16
<b>SEHEMU YA TATU .....</b>	<b>18</b>
<b>VIASHIRIA VYA RUSHWA, UDANGANYIFU NA UBADHIRIFU.....</b>	<b>18</b>
Jambo la 1: Uwezekano wa Serikali Kupoteza Mapato ya TZS 265.85 Bilioni .....	19
Jambo la 2: Matumizi yasiyo na tija TZS 380.92 bilioni katika Matumizi ya Kawaida .....	24
Jambo la 3: Matumizi ya TZS 1,124.07 bilioni katika Ununuzi wa Umma na Usimamizi wa Mikataba yanaviashiria vya Rushwa, Ubahirifupi na Udanganyifu.....	27
<b>HITIMISHO .....</b>	<b>31</b>

## UTANGULIZI

Ripoti ya Uwajibikaji ya Ufanisi, Rushwa na Ubadhirifu katika Sekta ya Umma ya mwaka 2021 imeandaliwa kutokana na ripoti 7 kati ya ripoti 15 za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) za ukaguzi wa Ufanisi za mwaka 2019/20 pamoja na kuchambua viashiria vya rushwa, udanganyifu na ubadhirifu katika ripoti za ukaguzi wa Serikali Kuu, Mashirika ya Umma, Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Miradi ya Maendeleo. Ripoti hizi 7 za ukaguzi wa ufanisi zimechambuliwa kwa kuwa zinawagusa wananchi moja kwa moja wakiwemo wanawake, vijana na watu wenye ulemavu katika nyanya za kiuchumi na kijamii.

Dhumuni la ripoti hii ni kurahisisha ripoti za CAG ili kuwawezesha wadau wa uwajibikaji kuelewa mapendekezo yaliyopo kwenye ripoti hizo na kudai uwajibikaji kutoka kwa watendaji wa Serikali (duty bearers) endapo uwajibikaji unaohitajika haupo. Ripoti hii itawawezesha wananchi (right holders) kuelewa namna rasilimali, mifumo na sera zilizopo zilivyotumika katika kuwaletaa maendeleo.

Wananchi wanaweza kutumia ripoti hii kama chanzo cha taarifa katika ufuutiliaji wa mapato na matumizi ya rasilimali za umma. Ufuutiliaji huo unaweza kutumia mbinu mbalimbali kama vile kuhoji kupitia vyombo vya habari, mikutano/midahalo na watendaji wa Serikali, kutumia nyenzo ya uwajibikaji jamii (SAM) au ufuutiliaji wa matumizi ya rasilimali za umma (PETS), kutoa taarifa na kushirikiana na TAKUKURU.

WAJIBU inatarajia ripoti hii itawakumbusha watendaji wa Serikali umuhimu wa kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa na CAG kwa madhumuni ya kuimarisha usimamizi wa rasilimali za Taifa. Mapendekezo yaliyomo katika ripoti hii yataisaidia Serikali kuboresha usimamizi wa rasilimali za taifa na utoaji huduma hivyo kuchochea kasi ya maendeleo ya nchi na wananchi wake.

Ripoti hii imegawanyika katika sehemu kuu nne (4): sehemu ya kwanza ni maana ya ukaguzi wa ufanisi na viashiria vya rushwa, udanganyifu na ubadhirifu; sehemu ya pili ni uchambuzi wa ripoti za ukaguzi wa ufanisi; sehemu ya tatu ni viashiria vya rushwa; udanganyifu na ubadhirifu na sehemu ya nne ni hitimisho.

Ripoti zilizochambuliwa ni Ripoti za Ukaguzi wa Ufanisi katika maeneo yafuatayo; Ufanisi wa Udhibiti wa Bei ya Uhamishaji Gharama (Transfer Pricing) nchini Tanzania kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania, Usimamizi wa Usafi katika Masoko ya Vyakula, Utekelezaji wa Mradi wa Uzalishaji Sukari Mbigiri Unaotekelezwa na Kampuni Tanzu ya Mkulazi Morogoro, Usimamizi na Ufuutiliaji wa Miradi Inayotekelezwa kwa utaratibu wa 'Force Account' katika Sekta ya Elimu, Usajili na Utoaji wa Vitambulisho vya Utaifa Unaotekelezwa na NIDA, Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA na Ripoti ya Ufuutiliaji wa mapendekezo ya CAG kwa ripoti tano za Ufanisi ziliizwasilishwa na kujadiliwa Bungeni Aprili, 2016.

Katika kufanya uchambuzi wa ripoti hizi, WAJIBU imezingatia mambo yafuatayo: changamoto zinazoikibili sekta iliyokaguliwa, mapungufu yanayoondoa ufanisi katika sekta iliyokaguliwa, athari zinazoweza kujitekeza kutokana na mapungufu hayo pamoja na kutoa ushauri wa nini kifanyike ili kuongeza ufanisi katika sekta husika.

Ripoti hii imeandaliwa na Taasisi ya WAJIBU kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Ujeruman (GIZ) nchini Tanzania kupitia Mradi wa Usimamizi Bora wa Fedha za Umma (GFG). Aidha, ripoti hii inasambazwa nchi nzima kwa ufadhili wa Ubalozi wa Ufalme wa Norway.

WAJIBU inawakaribisha wadau kuisoma ripoti hii na kutoa maoni yatakayochangia kuboresha ripoti zitakazofuata.

# SEHEMU YA KWANZA

## MAANA YA UKAGUZI WA UFANISI NA VIASHIRIA VYA RUSHWA, UDANGANYIFU NA UBADHIRIFU

Katika sehemu hii, ripoti imezungumzia maana ya ukaguzi wa ufanisi, viashiria vya rushwa, udanganyifu na ubahirifupi pamoja na vigezo viliviyotumika kubainisha maeneo hayo.

### Maana ya Ukaguzi wa Ufanisi

Ukaguzi wa ufanisi ambao pia hujulikana kama ukaguzi wa thamani ya fedha ni ukaguzi unaofanyika katika mifumo, sera na mipango mikakati mbalimbali ya taasisi ili kuona kama kuna thamani ya fedha na tija katika utekelezaji wake kwa kuzingatia uwekevu, tija na ufanisi. Uwekevu, tija na ufanisi vinaweza kuelezwa kama ifuatavyo:

- Uwekevu:** ni kupunguza ghamama za rasilimali zinazotumika katika shughuli kwa kuzingatia ubora unaohitajika.
- Ufanisi:** ni kiwango cha malengo yaliyofikiwa na uhusiano uliopo kati ya malengo yaliyokusudiwa na matokeo halisi yaliyofikiwa katika shughuli husika.
- Tija:** ni uhusiano uliopo kati ya matokeo yaliyopatikana kwa kuzingatia bidhaa, huduma na rasilimali zilizotumika kuzalisha matokeo hayo.

CAG hufanya ukaguzi wa thamani ya fedha kwa mujibu wa kifungu cha 28 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008 (na marekebisho yake). Tofauti na aina zingine za ukaguzi, ukaguzi wa thamani ya fedha haupelekei CAG kutoa Hati ya Ukaguzi, bali hutoa hitimisho na mapendekezo ya nini kifanyike ili kuongeza ufanisi. Ukaguzi huu unaweza kuhusisha taasisi zaidi ya moja kulingana na aina na idadi ya wadau au taasisi zinazohusika kwenye eneo linalokaguliwa.

### Maana ya Viashiria vya Rushwa, Udanganyifu na Ubahirifupi:

Rushwa, udanganyifu na ubahirifupi ni vitendo vinavyosababisha ufisadi. Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi ISA 240, ISSAI 1224 pamoja na ISSAI 1315 vinatoa maana ya udanganyifu au ufisadi kuwa ni “kitendo au vitendo vya makusudi vinavyofanywa na watu au mtu kwa ajili ya kupata faida kwa njia haramu au isiyo ya haki”.

Athari ya vitendo vya rushwa, udanganyifu na ubahirifupi ni pamoja na: upotetu wa fedha za umma, wananchi kutokuwa na imani na Serikali yao, kukosekana kwa utawala bora, uvurugaji wa bei ya soko kwa bidhaa mbalimbali na kupelekea wananchi kukosa huduma bora za kijamii.

### Vigezo Viliviyotumika Kubainisha Viashiria vya Rushwa, Udanganyifu na Ubahirifupi

Katika uchambuzi wa ripoti za CAG, yapo maeneo ambayo yanaonesha uwepo wa viashiria vya rushwa, udanganyifu na ubahirifupi. WAJIBU imetumia vigezo vifuatavyo katika kuainisha maeneo hayo:

- Mapato kutopelekwa benki,
- Kukosekana kwa hati za malipo,

- c) Kutumia hundi ya malipo iliyoghushiwa,
- d) Kwenda kinyume na Sheria, Kanuni na Taratibu za manunuzi na ulipaji fedha za umma,
- e) Kupokea huduma au bidhaa kwa uthibitisho wa uongo,
- f) Malipo ya huduma na bidhaa ambazo hazijatolewa au hazijapokelewa,
- g) Malipo kwa watumishi hewa,
- h) Matumizi mabaya ya nafasi au cheo katika kufanya maamuzi ya makusanyo na matumizi ya fedha za umma,
- i) Malipo kwa mkandarasi ambaye hajulikani au malipo yake hayajaidhinishwa,
- j) Kupokea huduma au bidhaa isiyo sahihi au ambayo haikukidhi viwango au mahitaji, na
- k) Kupokea huduma au bidhaa mbadala bila makubaliano halali.

Kwa kutumia vigezo vilivyoainishwa hapo juu, ripoti za CAG za mwaka 2019/20 zinaonesha kuwepo kwa matukio mbalimbali yanayoashiria rushwa, udanganyifu na ubahirifupi kama yalivyochambuliwa katika sehemu ya tatu ya ripoti hii.

# SEHEMU YA PILI

## UCHAMBUZI WA RIPOTI ZA UKAGUZI WA UFANISI

Sehemu hii imezungumzia mambo ambayo yamechambuliwa kutoka katika ripoti 7 za ufanisi kati ya ripoti 15 zilizotolewa mwaka 2021. Mambo hayo ni kama ifuatavyo;

### Jambo la 1: Mapungufu Kwenye Ufuatiliaji wa Miradi Iliyotekelawa kwa Utaratibu wa “Force Account” Katika Sekta ya Elimu

“Force account” ni utaratibu wa utekelezaji wa miradi ya ujenzi kupitia usimamizi wa wataalamu waliopo katika taasisi husika. CAG alibaini mapungufu yafuatayo katika utekelezaji wa miradi iliyotekelawa kwa utaratibu wa “force account” katika sekta ya elimu:

- a) Kukosekana kwa wataalamu wanaoweza kusimamia na kufutilia kitaalamu miradi inayotekelawa kwa utaratibu wa “force account” hususani kwenye kamati za shule. Mfano, kazi ya kusimamia miradi yenye thamani ya TZS 152.00 milioni mpaka TZS 259.00 milioni iliyotekelawa katika Halmashauri za Wilaya za Nzega, Nachingwea na Mpwapwa ilifanyanya na wahandisi wasio na sifa, hivyo kuwa na majengo yasiyo na kiwango kinachostahili hali inayoweza kuhatarisha maisha ya watumiaji wa majengo hayo na kusababisha kutokuwepo kwa thamani ya fedha ya miradi iliyotekelawa.
- b) Kutokumika kwa mfumo wa ununuzi wa umma (TANePS) katika utekelezaji wa miradi inayotumia utaratibu wa “force account”. Hii ni kutokana na Muongozo wa “force account” kutokuweka mkazo wa matumizi ya mfumo huo. Mfano; Watekelezaji wa miradi 23 iliyokaguliwa hawakutumia mfumo wa ununuzi wa umma wa TANePS.
- c) Wasimamizi wa miradi hawazingatii Sheria ya Ununuzi wa Umma (2011) na Aya ya 4 (1) ya Muongozo wa “force account” uliotolewa na OR-TAMISEMI unaozitaka taasisi zinazofanya manunuzi kuandaa takwimu za vifaa vitakavyotumika katika utekelezaji wa miradi. Mfano, taasisi nunuzi 23 hazikufanya majadiliano ya punguzo la bei kabla ya kusaini mkataba au kununua bidhaa.
- d) Baadhi ya majengo yaliyokamilika kutotumika kwa madhumuni yaliyokusudiwa. Mfano, Shule ya Sekondari ya Mwanzoli, iliyopo Nzega Mjini ilikuwa na vyumba viwili vya bweni vilivytumika kama stoo na mabweni mawili ambayo yamekamilika lakini hayatumiki. Pia, Shule ya Sekondari Kitangili, iliyopo Nzega Mjini ilikuwa na vyumba viwili vya madarasa pamoja na jengo la utawala ambayo yamekamilika lakini hayatumiki.

#### Athari:

Mapungufu yaliyobainishwa katika utekelezaji wa miradi kwa utaratibu wa “force account”, yamepelekea kuwepo kwa athari zifuatazo:

- a) Kuwepo kwa viashiria vya rushwa na udanganyifu katika mchakato wa ununuzi wa umma. Mfano; Kutilia shaka ushindani kwenye mchakato wa ununuzi katika miradi 21 yenye thamani ya TZS 2.13 bilioni inayotekelawa kwa utaratibu wa “force account”, kutokana na nyaraka za zabuni zilizowasilishwa kuwa na miandiko inayofanana na kutokua na muhuri wa mto huduma.

- b) Kuwepo kwa upotevu/ubahirifu wa fedha za umma. Mfano; Manunuzi yalifanyika kwa bei ya juu kuliko bei ya soko na kusababisha upotevu wa kiasi cha TZS 100.16 milioni ambazo zingeokolewa kama Sheria ya Ununuzi ya Umma 2016 kifungu 4A (3) (na marekebisho yake) ingezingatiwa.
- c) Kukosekana kwa thamani ya fedha katika miradi iliyotekelizwa. Mfano; Majengo kupata nyufa muda mfupi baada ya kukamilika katika Shule za Sekondari Berege na Mazae zilizopo H/W Mpwapwa na Shule ya Sekondari Bulunde iliyopo H/Mji Nzega.



#### Ushauri:

Ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa miradi kwa utaratibu wa "Force Account", WAJIBU inashauri yafuatayo:

- a) Mamlaka ya Udhhibit wa Ununuzi wa Umma (PPRA) iandae vigezo au mahitaji ya awali yatakayoziezesha Halmashauri kutekeleza miradi kwa utaratibu wa force account kikamilifu kisha ifanye tathimini ya uwezo wa Halmashauri zote nchini kama zinaweza kuendelea kutekeleza miradi kwa utaratibu huu.
- b) Halmashauri zitoe elimu ya ununuzi wa umma kwa wasimamizi wa miradi inayotekelizwa kwa utaratibu wa "force account" hususani kamati za shule ili kuongeza ufanisi katika miradi.
- c) Serikali iboreshe muundo wa utendaji katika ngazi ya kata ili kuongeza wataalamu watakapoishirikiana na Mtendaji wa Kata katika kusimamia miradi ya maendeleo. Baadhi ya wataalamu wanaokosekana katika ngazi ya kata ni kama vile Afisa TEHAMA, Mhasibu na Mhandisi.

## Jambo la 2: Udhaifu katika Mifumo ya TEHAMA

Serikali imejitahidi kutumia TEHAMA katika kuboresha usimamizi wa makusanyo na matumizi ya fedha za umma. Mifumo hii imelenga kuongeza udhibiti wa makusanyo ya fedha za umma, kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma za kijamii, kuongeza mapato na kuleta tija katika matumizi ya fedha za Umma. Hata hivyo, kumekuwa na changamoto mbalimbali zinazoikabili mifumo hii kama inavyoolezwa kwenye ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi katika mifumo ya TEHAMA ambapo CAG alibaini changamoto katika maeneo yafuatayo:

### i. **Udhaifu wa Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya TEHAMA ya mwaka 2016**

Sera ya Taifa ya TEHAMA ya mwaka 2016, inazitaka taasisi zote za umma nchini kuandaa Sera na Mpango Mkakati wa TEHAMA utakaoziongoza katika matumizi ya TEHAMA. Ukaguzi wa CAG ulibaini kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa 18 pamoja na baadhi ya taasisi za Serikali hazina Sera na Mipango Mikakati ya mifumo ya TEHAMA. Pia, sera na mipango mikakati iliyopo haiendani na kanuni za fedha katika taasisi zilizokaguliwa. Baadhi ya taasisi zilizobainishwa kuwa na changamoto hiyo ni: Kampuni ya Uendelezaji wa Jotoardhi Tanzania (TGDC), Kituo cha Mahusiano ya Kigeni (CFR), Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA), Shirika la Usimamizi na Ukaguzi wa Ushirika (COASCO), Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) na Mamlaka ya Maji Singida (SUWASA).

### ii. **Kukosekana kwa Ufanisi katika Utendaji wa Mifumo ya TEHAMA**

CAG alibaini mapungufu mbalimbali yanayoondoa ufanisi katika utendaji wa mifumo ya TEHAMA kama ifuatavyo:

#### **■ Mfumo wa manunuzi wa Kieletroniki (TANePS)**

Ukaguzi ulibaini kuwa muuzaji wa mfumo huu hakuiwezesha Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) kuifikia seva (server) na kanzi-data ya TANePS. Hivyo, PPRA haiwezi kufuatilia shughuli zinazofanywa na muuzaji wa mfumo huu au kugundua shughuli zisizoruhusiwa katika seva na kanzi-data. Aidha, mfumo wa TANePS hauna uwezo wa kutoa taarifa kuhusu jumla ya taasisi zinazofanya manunuzi nchini, idadi ya taasisi ambazo hazikuwasilisha mpango wa manunuzi wa mwaka na idadi ya mikataba ya manunuzi iliyotekerezwa katika kiwango cha nchi au kitaasisi.

Vilevile, mfumo wa TANePS haujaunganishwa na mifumo mingine ya Serikali mfano: Mfumo wa Bajeti wa Serikali Kuu (CBMS); Mfumo wa Matumizi na Malipo ya Serikali (MUSE); Mfumo unaotumika kutambua wazabuni wenye sifa (GPSA); Mfumo wa Malipo ya Serikali (GePG) na Mfumo wa kupanga bajeti na kutoa ripoti za utekelezaji katika Halmashauri (PlanRep). Kutounganishwa kwa mifumo hii, ni kinyume na dhana ya kuwa na mifumo ya TEHAMA ambayo inarahisisha kazi na badala yake kufanya kazi kuwa ngumu na zenye mlolongo mrefu wa kiutendaji.

#### **■ Mfumo wa Bajeti wa Serikali Kuu (CBMS)**

Mfumo huu hauwezi kuzuia uwasilishaji wa bajeti iliyozidi kiwango kilichoidhinishwa. Pia, mfumo haumwezeshi Afisa Masuuli (Mtendaji Mkuu) kuidhinisha bajeti kabla haijawasilishwa Wizara ya Fedha na Mipango na hauna udhibiti wa kutosha katika usimamizi wa utekelezaji wa bajeti iliyoidhinishwa.

## ■ Mfumo wa Ukusanyaji wa Mapato Serikali za Mitaa (LGRCIS)

Mapungufu yaliyobainishwa katika mfumo huo ni pamoja na:

- Kushindwa kukokotoa ushuru wa huduma, ada za ujenzi wa majengo na adhabu,
- Kushindwa kuonesha kiasi sahihi cha fedha ambazo hazijawasilishwa benki,
- Kukosekana kwa uwiano wa muda wa leseni za biashara unaooneshwa katika mfumo na katika kanuni za leseni ya biashara,
- Kushindwa kutunza kumbukumbu za miamala ya makusanyo katika mashine za kukusanya mapato (POS) zilizopotea ama kuharibika, na
- Uwezekano wa kuvuruga taarifa za mashine hizo kutokana na udhaifu wa udhibiti wa kielektroniki.

### iii. Uwepo wa Mifumo ya TEHAMA Inayofanya Kazi Zinazofanana

Kuweipo kwa mifumo inayofanya kazi zinazofanana ni dalili ya kutokuwepo kwa mawasiliano thabiti ya kiutendaji kati ya Wizara, Idara na Taasisi za Serikali. CAG alibaini uwepo wa baadhi ya mifumo tofauti ya TEHAMA inayofanya kazi zinazofanana kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 1.

**Jedwali 1: Mifumo ya TEHAMA Inayofanya Kazi Zinazofanana**

Mfumo A	Mfumo B	Kazi zinazofanana
PlanRep: Mfumo unaotumika katika kupanga, kubajeti na kutoa ripoti za utekelezaji katika Halmashauri.	TiMES: Mfumo jumuishi wa ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa bajeti katika Halmashauri.	Hii ni mifumo miwili tofauti ambayo inatumika kwa usimamizi wa utekelezaji wa bajeti ngazi ya Halmashauri.
IFT - MIS: Mfumo unaofuatilia utekelezaji wa mapendekezo na maagizo ya CAG, PPRA na LAAC.	GARI-ITS: Mfumo unaofuatilia utekelezaji wa Mapendekezo ya kaguzi za Serikali.	Hii ni mifumo miwili tofauti ambayo inatumika kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo ya CAG, PPRA na LAAC katika ngazi ya Halmashauri.
SIS: Mfumo unaotumika kukusanya takwimu za shule kama vile mahudhurio ya wanafunzi na maendeleo, idadi ya wanafunzi, walimu, na vitabu.	ASC: Mfumo unaotumika kukusanya takwimu kutoka shule za msingi, sekondari, na elimu ya watu wazima.	Hii ni mifumo miwili tofauti ambayo inatumika kukusanya takwimu za shule.

**Athari:**

Udhafu uliobainishwa kwenye mifumo hii una athari zifuatazo;

- a) Kutokuwepo kwa sera na mipango mikakati mizuri inayoendana na mahitaji ya TEHAMA kwa wakati kumesababisha kukosekana kwa ufanisi wa matumizi ya TEHAMA serikalini hivyo kushindwa kurahisisha utendaji na utoaji huduma kwa wananchi.
- b) Changamoto za kimfumo zinaongeza uwezekano wa watumishi wasio waadilifu kufanya vitendo vyta ulaghai na hivyo kutumia vibaya mapato wanayoyakusanya. Mfano, katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbanga, Afisa TEHAMA na Mhasibu Msaidizi walikuwa na mashine yao ya kukusanya mapato ambayo yalikuwa hayaonekani kwenye mfumo wa LGRCIS na taarifa zake zilikuwa haziendi kwenye mfumo wa mapato hivyo kufanikiwa kukusanya na kuiba TZS 270.05 milioni.
- c) Bajeti kutotumika kama nyenzo ya udhibiti (control tool) kulikopelekea fedha kutumika zaidi ya viwango vilivyoidhinishwa na Bunge. Mfano: CAG alibaini taasisi sita zilizopo chini ya Wizara mbalimbali zilifanya matumizi yenye jumla ya TZS 24.41 bilioni ambayo hayakuwa kwenye bajeti kinyume na Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015.
- d) Kuwepo kwa mifumo miwili au zaidi inayofanya kazi zinazofanana kunaongeza gharama za uendeshaji na matengenezo ya mifumo ya TEHAMA inayotumiwa na Serikali.
- e) Kukosekana kwa muingiliano (lack of interlink) baina ya mifumo ya TEHAMA inayotumiwa Serikalini kunaongeza mianya ya wizi na ubahirifupi wa fedha za umma.

**Ushauri:**

Katika kutatua changamoto zilizowasilishwa hapo juu, WAJIBU inashauri Serikali ichukue hatua zifuatazo;

- a) Mamlaka ya Serikali Mtando (eGA) kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango ifanye mapitio ya mifumo yote ya TEHAMA inayohusika katika usimamizi wa makusanyo na matumizi ya fedha za umma ili;
  - i. Kuunganisha mifumo inayofanya kazi zinazofanana (PlanRep dhidi ya TiMES, IFT-MIS dhidi ya GARI-ITS na SIS dhidi ya ASC) na kutengeneza moduli ambazo hazipo katika mifumo hiyo,
  - ii. Kuunganisha mifumo ambayo haiwasiliani (TANePS na mifumo ya MUSE, PLANREP, CBMS na GPSA),
  - iii. Kuongeza udhibiti wa matumizi ya mifumo ya TEHAMA (mfano, LGRCIS) na
  - iv. Kuhakikisha seva na kanzi data ya mifumo (mfano, TANePS), zinamilikiwa, zinaendeshwa na zinasimamiwa na taasisi za serikali na sio watu au taasisi binafsi.



- b) TAKUKURU kufanya uchunguzi na kuwafikisha mahakamani watendaji wanaotuhumiwa kwa vitendo vya rushwa, udanganyifu na ubadhirifu katika mifumo ya usimamizi wa makusanyo na matumizi ya fedha za umma.

### Jambo la 3: Utilewaji wa Vitambulisho vya Taifa Usioridhisha


Tangu lilipoanza zoezi la utilewaji wa vitambulisho vya Taifa mwaka 2012/13, ni wananchi 5,621,350 tu ndio waliopata vitambulisho vya Taifa sawa na asilimia 26 ya wananchi 21,692,122 walioandikishwa NIDA hadi kufikia Juni, 2020. Zoezi la usajili na utoaji wa vitambulisho vya Taifa kwa wananchi, linaathiriwa na sababu zifuatazo:

- Mwaka 2016/17 Serikali iliagiza vitambulisho vya taifa viwe na saini ya mwenye kitambulisho, hatua ambayo ilipelekea uwezo wa mashine katika uzalishaji vitambulisho kushuka kutoka vitambulisho 3,168,000 hadi vitambulisho 1,584,000 kwa mwaka. Kutokana na kuweka saini katika vitambulisho pamoja na kutokuwepo kwa matengenezo ya mashine za kuzalisha vitambulisho imepelekea NIDA kuzalisha idadi ndogo ya vitambulisho kulinganisha na uwezo wa mashine zilizopo.
- Ufinyu wa idadi ya watumishi katika ofisi za Wilaya: CAG alibaini, asilimia 38 ya Wilaya 150 zilikuwa na watumishi watatu wakati asilimia 62 zilikuwa na watumishi 2. Kwa kila Wilaya kunatakiwa kuwe na watumishi kuanzia watatu wanaofanya utambuzi, usajili na ugawaji wa vitambulisho lakini imekuwa kinyume na utaratibu wa NIDA. Mfano, Halmashauri ya Wilaya za

Mbarali, Malinyi, Sumbawanga, Namtumbo, Itilima na Momba kila Halmashauri ina mtumishi mmoja tu anayefanya zoezi la usajili na utoaji wa vitambulisho.

- c) Kutokutumika kwa Mashine mbili zenyne thamani ya TZS 10.05 bilioni zilizokuwa na uwezo wa kutoa vitambulisho 19,008,000 kwa mwaka ingawa watumishi wanne walipewa mafunzo ya kutumia mashine hizo.
- d) Uchapaji mdogo wa vitambulisho ikilinganishwa na wingi wa wananchi walioandikishwa kama inavyoonekana kwenye kielelezo Na. 1.

#### Kielelezo 1: Idadi ya Wananchi Waliopata Vitambulisho vya Taifa (TZS Milioni)




#### Athari:

Athari za changamoto zilizotolewa hapo juu ni kushindwa kwa NIDA kutoa vitambulisho kwa wakati na kupelekea wananchi kukosa huduma hii stahiki na kutokuwepo kwa thamani ya fedha kwa fedha zilizowekezwa kwenye mradi huu. Mfano: kushindwa kupata hati ya kusafiria (pasipoti), kushindwa kusajili kadi za simu za mkononi, kukosa baadhi ya huduma za kifedha na kibia shara. Hali hii imesababishia watu 16.07 milioni sawa na asilimia 67 ya wananchi waliosajiliwa kutopata vitambulisho licha ya Serikali kutumia kiasi cha TZS 148.80 bilioni kwa kipindi cha miaka mitano kwenye mradi huu (2015/16-2019/20).

## TZs 10.05 billioni

Thamani ya mashine mbili ambazo zina uwezo wa kutoa vitambulisho **19,008,000** kwa mwaka.



#### **Ushauri:**


WAJIBU inaishauri Serikali kuitia ofisi ya Waziri Mkuu kufanya mapitio ya kina juu ya muundo na mfumo wote wa kiutendaji wa NIDA ili kufanya mabadiliko yatakayoweza kuondoa changamoto za utoaji wa vitambulisho ambazo zimedumu tangu kuanzishwa kwa mradi huu wa vitambulisho ya Taifa tangu mwaka 2012/13.

#### **Jambo la 4: Uchakavu na Uchafu katika Masoko ya Chakula**

Masoko ya chakula nchini yamekuwa katika hali ya uchakavu na uchafu hivyo kuhatarisha afya za watumiaji wa huduma za masoko hayo hususani wanawake ambao ndio watumiaji wakubwa wa huduma hii. Hii ni kinyume na Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 (kama iliyorekebiswa) inayozipa Mamlaka ya Serikali za Mitaa jukumu la kusimamia na kuboresha Afya ya Jamii. Sababu zinazopelekea uchafu na uchakavu katika masoko hayo ni kama ifuatavyo:


- Agizo la Ofisi ya Rais – TAMISEMI, linataka kila Halmashauri kutenga asilimia 15 ya mapato yanayopatikana kutoka katika masoko ili kutekeleza shughuli za maendeleo, marekebisho na usafi katika masoko hayo. Hata hivyo, Halmashauri 8 zilishindwa kutenga asilimia 15 ya kiasi cha fedha kinachokusanywa kama mapato kutoka katika masoko ili kugharamia usafi wa masoko hayo. Mfano, Halmashauri ya Manispaa ya Ilala ilitenga asilimia 5, wakati Halmashauri ya Jiji la Dodoma na Mbeya, Manispaa za Kigoma Ujiji na Temeke na Wilaya za Korogwe, Mbarali na Sengerema hazikutenga kiasi chochote cha fedha kwa ajili hiyo katika kipindi cha miaka minne (2016/17 – 2019/20) kama inavyoonekana katika kielelezo Na. 2.

**Kielelezo Na 2: Jumla ya Fedha Zilizokusanywa Kutoka katika Masoko ya Chakula na Fedha Zilizorudishwa ili Kugharamia Usafi wa Masoko Hayo kwa Kipindi cha Miaka Minne (2016/17 - 2019/20)**



- ii. Katika ukaguzi huo, CAG alibaini masoko 8 kati ya masoko 20 yaliyotembelewa, hayakuwa na watoa huduma waliosajiliwa kutoa huduma mbalimbali ikiwemo huduma za kuondoa takataka na kufanya usafi katika maeneo ya soko. Vilevile, CAG alibaini kuwepo kwa idadi kubwa ya wafanyabiashara katika masoko zaidi ya uwezo wa masoko hayo kama inavyoonekana katika kielelezo Na. 3, ambapo hali hii husababisha uzalishaji mkubwa wa takataka na uchakavu wa miundombinu.

**Kielelezo Na 3: Asilimia ya Idadi ya Wafanyabiashara waliozidi katika masoko ya chakula ukilinganisha na uwezo wa soko**




- iii. CAG alibaini kulikuwa na udhaifu katika usimamizi wa uendeshaji wa masoko ambapo kati ya Halmashauri 10 zilizokaguliwa, Halmashauri 5 hazikuwa na sheria ndogondogo za usimamizi wa usafi wa masoko. Pia, Halmashauri 7 kati ya 10 hazikuwa na miongozo ya kusimamia kamati za usimamizi wa masoko kwenye masuala ya usafi. Masoko 14 kati ya 25 yaliyokaguliwa hayakuwa na kamati za usimamizi wa masoko pamoja na kutokuwa na uongozi wa masoko yaliyokuwepo.

#### Athari:

Kutokana na mapungufu yaliyobainishwa, athari zilizojoitokeza katika masoko ya chakula 25 yaliyokaguliwa ni kama zifuatazo:

#### Athari zilizojoitokeza:



Mapungufu yaliyobainishwa yamesababisha wananchi kuendelea kununua vyakula katika masoko ambayo si salama kiafya. Masoko hayo yanaweza kusababisha milipuko ya magonjwa yanayotokana na uchafu kama vile kipindupindu. Vilevile, Uchakavu wa miundombinu huathiri zaidi wafanyabiashara wa jinsi ya kike ambao ndio watumiaji wakubwa wa masoko ya chakula kwa kukosa maeneo bora ya kujisitiri na kufanya biashara.

#### Ushauri:

WAJIBU inashauri OR - TAMISEMI kuhimiza Halmashauri zote nchini kuhakikisha kuwa zinafuata agizo linalowataka kutenga asilimia 15 ya mapato yanayopatikana katika masoko ili kutekeleza shughuli za maendeleo, marekebisho na usafi katika masoko yao. Vilevile, OR - TAMISEMI iwachukulie hatua za kinidhamu watendaji wote wa Halmashauri ambao hawatatenga asilimia 15 ya mapato yanayopatikana katika masoko ili kutekeleza shughuli za maendeleo, marekebisho na usafi katika masoko. Pia, Halmashauri zitakiwe kusimamia kikamilifu uanzishwaji wa kamati za usimamizi wa masoko, utungaji wa sheria ndogondogo za usimamizi wa usafi wa masoko na uimarishaji, ufuutiliaji wa uendeshaji wa masoko.

### Jambo la 5: Mapungufu katika Ukusanyaji wa Kodi ya “Uhamishaji Gharama” ya Mauziano

CAG alibaini mapungufu katika kusimamia ukusanyaji kodi katika miamala ya uhamishaji gharama (transfer pricing) katika mauziano baina ya taasisi zenyе uhusiano wa kimataifa (multinational corporations). Miamala ya uhamishaji gharama (transfer pricing), hutokeea pale ambapo kampuni iliyoko ndani ya nchi inafanya biashara na kampuni ilio nje ya nchi. Kutokana na tofauti ya viwango vya kodi kati ya nchi na nchi, wafanya biashara hao hushawishika kuongeza au kupunguza gharama za mauziano baina yao ili kuhamishia kiasi kikubwa cha faida katika nchi yenye unafuu wa kodi. Kupitia njia hii makampuni mengi hukwepa kodi ambazo wangepaswa kulipa nchini kutokana na kuonesha gharama kubwa za ununuzi wa huduma na bidhaa nje ya nchi na kupelekea kuwa na hasara katika biashara zinazofanyika hapa nchini. Baadhi ya mapungufu yaliyobainika katika usimamizi wa kodi zinazotokana na miamala ya uhamishaji gharama ni kama ifuatavyo:

- Kukosekana kwa Sera na Mkakati maalumu wa kusimamia uhamishaji gharama katika mauziano baina ya kampuni zenyе uhusiano wa kimataifa. Mfano; kwa kipindi cha miaka minne (2016/17 - 2019/20), ni makampuni 60 sawa na asilimia 11.9 tu ndiyo yaliyokaguliwa katи ya makampuni ya kimataifa 504 yaliyotakiwa kufanyiwa ukaguzi wa miamala ya uhamishaji gharama (transfer pricing audit). Hii ni kutokana na kukosekana kwa sera na mpango unaozingatia vihatarishi vya ukwepaji kodi kupitia uhamishaji gharama katika mauziano baina ya kampuni zenyе uhusiano wa kimataifa.
- Uwezo mdogo wa watumishi na uhaba wa vitendea kazi katika usimamizi, utekelezaji na ufuatiliaji wa miamala ya uhamishaji gharama. Mfano; kwa kipindi cha miaka minne (2016/17 - 2019/20), TRA ilitarajia kufanya kaguzi zilizopangwa na kaguzi za dharura 180 katika miamala ya uhamishaji gharama. Hata hivyo, TRA ilianzisha kaguzi 60 sawa na asilimia 33 ambapo katи ya kaguzi hizo 60 ni kaguzi 23 sawa na asilimia 38 ndizo zilifanyika kikamilifu.
- Ufinyu wa bajeti katika kitengo cha usimamizi wa uhamishaji gharama inayotokana na mauziano baina ya kampuni zenyе uhusiano wa kimataifa. Mfano; Serikali imekuwa ikitoa kiasi kidogo cha bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya Kitengo cha Kodi za Kimataifa kama inavyoonekana kwenye jedwali Na. 2

### Jedwali Na 2: Mtiririko wa bajeti iliyoidhinishwa na fedha iliyotolewa katika Kitengo cha Kodi za Kimataifa kwa kipindi cha miaka minne (2016/17 – 2019/20)

MWAKA	BAJETI ILIYOIDHINISHWA (TZS MILIONI)	FEDHA ZILIZOTOLEWA (TZS MILIONI)	FEDHA ZILIZOTOLEWA (%)
2016/17	3,699.91	95.87	3
2017/18	2,727.22	308.88	11
2018/19	2,862.92	552.44	19
2019/20	3,469.10	689.21	20
<b>JUMLA</b>	<b>12,759.15</b>	<b>1,646.40</b>	<b>13</b>

Kwa hali hii ya utoaji fedha za uendeshaji wa Kitengo cha Kodi za Kimataifa kwa asilimia 3 hadi 29 hukwamisha ufanisi wa kitengo hicho.

- d) Sekta muhimu zenyenye mchango mkubwa katika uchumi wa nchi kama vile kilimo inayochangia asilimia 27.7, ujenzi asilimia 13.6, uzidua jisilimia 5 na viwanda asilimia 4, hazikuhusishwa kwenye mpango wa ukaguzi wa miamala ya uhamishaji gharama kutokana na ukosefu wa kanzidata.
- e) Changamoto za ubadilishanaji wa taarifa za kodi. Kwa kipindi cha miaka minne (2016/17 - 2019/20) TRA ilipanga kuanzisha mazungumzo ya mikataba au kupitia mikataba 12 ya kubadilishana taarifa za fedha na faida za makampuni yanayofanya biashara ndani na nje ya nchi kila mwaka ili kuiwezesha mamlaka kufanya ulinganifu, lakini haikufanya mazungumzo hayo kutokana na uwepo wa sheria zinazozua mabadilishano ya taarifa za nchi na wadau wa kimataifa. Hii ni kinyume na Kanuni ya 6 (5) ya Kanuni za Usimamizi wa Kodi ya mwaka 2018.

#### **Athari:**

Kutokana na mapungufu yaliyobainishwa, athari zilizojitokeza katika kusimamia ukusanyaji kodi katika miamala ya uhamishaji gharama ni kama zifuatazo:

- a) Kutokana na utekelezaji duni wa ukaguzi wa miamala ya uhamishaji gharama, ripoti za mwaka za utendaji za TRA zinaonesha ongezeko la kodi la TZS 27.34 bilioni kutoka katika kodi ya TZS 53.66 bilioni iliyoripotiva na makampuni mwaka 2017/18. Hivyo, kama kungekuwa na ufanisi katika kusimamia eneo hilo, Serikali ingeweza kukusanya kiasi kikubwa zaidi kutoka katika kesi za kodi zenyenye thamani ya TZS 1.03 triliioni kwa mwaka 2018/19 na 2019/20 na kuiwezesha Serikali kutekeleza miradi mingi zaidi ya maendeleo.
- b) Serikali kushindwa kupata taarifa halisi za bei zilizopo sokoni kutokana na ukosefu wa mikataba ya mabadilishano ya taarifa za kodi baina ya nchi na nchi, hivyo kuchangia ukwepajji kodi kwa makampuni yenye mahusiano ya kimataifa.

#### **Ushauri:**

WAJIBU inashauri Wizara ya Fedha na Mipango kwa kushirikiana na TRA ziandae Sera na Mkakati maalumu wa usimamizi na ufuatiliaji wa miamala ya uhamishaji gharama. Vilevile, zitoe bajeti yote inayoidhinishwa ya kitengo cha kodi za kimataifa (ITU) ili kusimamia utekelezaji na ufuatiliaji wa makampuni yanayofanya miamala ya uhamishaji gharama ili kuhakikisha kodi stahiki inakusanywa.

Vilevile, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali iisimamie Serikali kuanzisha na kukamilisha mazungumzo na makubaliano yote ya ubadilishanaji wa taarifa kati ya Tanzania na nchi mbalimbali kama inavyoonesha katika mpango mkakati wa Mamlaka ya Mapato Tanzania. Hii ni pamoja na Bunge kufanya mapitio ya sheria zote zinazozua Mamlaka ya Mapato Tanzania kufanya mabadilishano ya taarifa za kodi baina yake na nchi mbalimbali.

#### **Jambo la 6: Utekelezaji Usioridhisha wa Mradi wa Uzalishaji wa Sukari Mbigiri**

Mradi wa Uzalishaji wa Sukari Mbigiri ambao unamilikiwa na kampuni tanzu ya Mkulazi uliyopo Wilayani Kilosa, Mkoani Morogoro una lengo la kuzalisha sukari tani 50,000 kwa mwaka. CAG alibaini mapungufu katika utekelezaji wa mradi huu kama ifuatavyo;

- a) Kampuni ya Mkulazi kushindwa kusimika mtambo wa kuchakata sukari kwa wakati. Hii ni kinyume na mkataba wa mwaka 2018 uliosainiwa kati ya kampuni ya Mkulazi, Benki ya Azania na Chama cha Ushirika cha Kati cha Magole uliokuwa na lengo la kukuza mnyororo wa thamani wa sukari kwa kuanzisha mahusiano baina ya wakulima, benki na kampuni. Kulunganana na mkataba, kampuni ya Mkulazi ilitakiwa kusimika mtambo wa kuchakata sukari ili benki iweze kutoa mkopo kwa wakulima. Hadi mwezi Disemba 2020, kampuni ya Mkulazi ilikuwa haijasimika mtambo huo wakati wakulima walikuwa wameshaanza kulima miwa na imesha komaa kwa matumizi ya utengenezaji wa sukari.
- b) Kampuni ya Mkulazi haikuweza kusimamia utendaji wa wakulima wanaouzunguka mradi kwa kuwapatia ushauri wa kiutaaalamu ili kuhakikisha uwepo wa miwa ya kutosha na yenye ubora kwa ajili ya kiwanda. Hii ni kinyume na Sera ya kilimo ya mwaka 2013 inayotaka kila unapofanyika uwekezaji mkubwa wa Kilimo kuhakikisha kwamba unawanufaisha wananchi wa eneo linalozunguka uwekezaji huo.

**Athari:**

Kutokana na usimamizi duni wa Mradi wa Mbigiri, wakulima kupitia vyama vyao vyaa msingi wameshindwa kufikia malengo walijojiwekea katika uzalishaji wa miwa kutokana na kupoteza fursa ya mkopo wa TZS 1.80 bilioni kutoka benki ya Azania. Mfano: kwa mwaka wa fedha 2017/18 lengo walijojiwekea lilikuwa kulima na kupanda ekari 3,200 za miwa lakini walifanikiwa kulima na kupanda ekari 1,044 tu za miwa. Kwa mwaka wa fedha 2019/20, lengo lilikuwa kupanda ekari 2,500 lakini walifanikiwa kulima na kupanda ekari 1,035 tu. Aidha, wakulima walishindwa kuvuna na kuuza miwa japokuwa walikuwa na mkataba wa kuuza miwa kwa Mradi wa Mbigiri. Hivyo, wakulima hao walisababishiwa kushindwa kumudu gharama za kuandaa mashamba, kunununa mbolea na dawa za wadudu, mbegu pamoja na kuchimba visima katika mashamba yao kwa msimu ujao.

Pia, kampuni ya Mkulazi imepoteza fedha kiasi cha TZS 11.64 bilioni sawa na asilimia 5 ya uwekezaji wote wa mradi kutokana na matumizi yasiyo na tija na usimamizi duni wa mradi.

**Ushauri:**

Ili kuzuia hasara inayoendelea kutokea katika mradi huu, WAJIBU inashauri yafuatayo:

- a) TAKUKURU iufanyie uchunguzi wa kina Mradi wa Mbigiri unaotekelizwa kupitia Kampuni tanzu ya Mkulazi ili kuokoa fedha na mali ambazo zinaendelea kupotea katika shamba la Mbigiri.
- b) Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) iwachukulie hatua za kinidhamu watendaji waliosababisha kasoro zilizojiteza pamoja na kutokutekeleza mapendekezo ya CAG yaliyotolewa mwaka 2018/19 yaliyolenga kuboresha uendeshaji wa mradi huu.
- c) Serikali inapoamua kuanzisha miradi ya aina hii, ihakikishe inafanya maandalizi ya kutosha ikiwepo kufanya upembuzi yakinitu na kufuata mpango mkakati uliowekwa ili kuhakikisha utekelezaji unakwenda kama uliyopangwa. Umuhimu huu unatokana na miradi ya aina hii kuhusisha sekta binafsi hivyo kunapotokea kulegalega kwa utekelezaji wake, huathiri zaidi uwekezaji wa sekta binafsi na kuendeleza mnyororo wa umaskini katika nchi.

- d) Serikali ifanye tathimini ya hasara ambayo wakulima wa miwa wamepata kutokana na kutokufanya kazi kwa mradi wa mbigiri na kuwalipa wakulima hao ili wawzeze kuendelea na mradi huo mara utakapo tengamaa.


#### **Jambo la 7: Utekelezaji wa Mapendekezo Yaliyotolewa Katika Baadhi ya Kaguzi za Ufanisi za Mwaka 2016:**

Mwaka 2019/20, CAG alifanya ukaguzi wa ufuatilaji wa utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti tano zilizotolewa Aprili 2016 ambazo ni;

- i. Usimamizi wa utoaji leseni na mikataba ya utafutaji na uendelezaji gesi asilia,
- ii. Ufuatilaji wa utekelezaji na uzingatiaji wa Sera, Sheria na Kanuni kwenye shughuli za utafutaji wa petroli Tanzania,
- iii. Utekelezaji wa matakwa ya maudhui ya ndani na uthibitisho wa gharama za uwekezaji katika mikataba ya uchangiaji wa gharama za uzalishaji,
- iv. Usimamizi wa taarifa za kijiografia na kijiolojia katika sekta ya mafuta na gesi asilia Tanzania, na
- v. Usimamizi wa uendelezaji rasilimaliwatu katika sekta ya mafuta na gesi asilia.

Ripoti hizo ziliwa na jumla ya mapendekezo 63 yaliyotakiwa kutekelezwa na taasisi 4 zinazosimamia utafutaji na uendelezaji wa mafuta na gesi asilia. Kati ya mapendekezo 63, ni mapendekezo 9 sawa na asilimia 14 ndio yaliyotekelizwa kikamilifu, mapendekezo 38 sawa na asilimia 60 yako kwenye hatua mbalimbali za utekelezaji, mapendekezo 13 sawa na asilimia 24 hayajatekelezwa kabisa na pendekezo 1 sawa na asilimia 2 limepitwa na wakati. Hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya CAG yaliyotokana na ripoti hizo ni kama inavyoonekana kwenye kielelezo Na. 4.

#### **Kielelezo Na 4: Utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na CAG kutokana na ripoti tano (5) za mwaka 2016.**



Taasisi ya PURA ndiyo inayoongoza kwa kutekeleza kikamilifu mapendekezo mengi yaliyotolewa na CAG kwa kuwa imetekeleza kikamilifu mapendekezo 7 sawa na asilimia 29 ya mapendekezo 24. Wizara ya Nishati inaongoza kwa kutotekeleza mapendekezo 11 sawa na asilimia 46 ya mapendekezo 24. NEMC ilikuwa ikiendelea na utekelezaji wa mapendekezo 10 sawa na asilimia 91 ya mapendekezo 11 yaliyotolewa.

#### **Athari:**

Kutotekelezwa kikamilifu kwa mapendekezo ya CAG kunaendelea kuathiri sekta ya nishati ikiwemo mfumo wa usimamizi wa utoaji wa mikataba na leseni za utafutaji na uendelezaji wa gesi asilia nchini. Hali hii, iliathiri maeneo ya tathmini ya uhitaji; maandalizi ya vigezo mahsus vy zabuni; utangazaji wa zabuni; tathmini ya zabuni zilizopokelewa. Eneo lingine linaloathirika zaidi ni eneo la majadiliano baina ya Serikali na wawekezaji kabla ya kutoa zabuni na kupelekea Serikali kushindwa kuingia mikataba na wawekezaji wa utafutaji na uendelezaji wa gesi asilia. Kutosainiwa kwa mikataba ya utafutaji na uendelezaji wa gesi asilia, kunaisababishia Serikali kukosa mapato kupitia mikataba na leseni ya uendelezaji wa gesi asilia hivyo kushindwa kutoa huduma za kijamii.



#### **Ushauri:**

WAJIBU inasisitiza umuhimu wa wahuksika kutekeleza kikamilifu mapendekezo ya CAG. Pia, AZAKI zinazofanya uchechemuzi katika sekta ya mafuta na gesi asilia na wananchi, kuendelea kudai utekelezaji wa mapendekezo ya CAG.

# SEHEMU YA TATU

## VIASHIRIA VYA RUSHWA, UDANGANYIFU NA UBADHIRIFU

Katika uchambuzi wa ripoti za CAG za mwaka 2019/20, WAJIBU imemeanisha maeneo yenye viashiria vya rushwa, udanganyifu na ubahirifupi wa fedha za umma. Kiasi ambacho aidha hakikukusanywa au kimetumika na Serikali pasipo kupata tija yoyote kimeongezeka kutoka TZS 232.52 bilioni mwaka 2018/19 hadi TZS 1,770.84 bilioni mwaka 2019/20. Mamlaka ya Serikali za Mitaa ndizo zimekuwa na ongezeko kubwa zaidi kutoka TZS 103.93 bilioni mwaka 2018/19 hadi TZS 863.85 bilioni kwa mwaka 2019/20 kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 3.

**Jedwali Na 3: Mwenendo wa Kiasi cha Makusanyo na Matumizi yenye Viashiria vya Rushwa, Udanganyifu na Ubahirifupi kwa Kipindi cha Miaka Mitatu (2017/18 - 2019/20)**

	2017/18	2018/19	2019/20
<b>TZS Bilioni</b>			
Jumla	207.12	232.52	1,770.84
Serikali Kuu	105.33	34.3	560.19
Mamlaka za Serikali za Mitaa	73.97	103.93	863.85
Mashirika ya Umma	27.82	94.29	346.80

### Ufunguo:

- Kiasi ni kidogo ukilinganisha na mwaka uliopita ama unaofuata
- Kiasi ni kikubwa ukilinganisha na mwaka uliopita ama unaofuata

Kati ya makusanyo na matumizi ambayo yanaviashiria vya rushwa, udanganyifu na ubahirifupi kwa mwaka 2019/20, Mamlaka ya Serikali za Mitaa ilikuwa na TZS 863.85 bilioni sawa na asilimia 49 ya TZS 1,770.84 bilioni ambapo kasoro nyingi zilioneekana katika eneo la ununuzi wa umma na usimamizi wa mikataba.

**Jedwali Na 4: Mchanganuo wa maeneo ambayo yanaviashiria vya rushwa, udanganyifu na ubahirifupi katika Serikali Kuu, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mashirika ya Umma kwa mwaka 2019/20**

	Serikali Kuu	Serikali za Mitaa	Mashirika ya Umma	Jumla	Asilimia (%)
<b>TZS Bilioni</b>					
Jambo la 1: Serikali yapoteza mapato ya TZS 265.85 bilioni	38.70	191.20	35.96	265.85	15
Jambo la 2: Matumizi yasiyo na tija TZS 380.92 bilioni katika matumizi ya kawaida	104.60	82.21	194.11	380.92	22
Jambo la 3: Matumizi ya TZS 1,124.07 bilioni katika ununuzi wa umma na usimamizi wa mikataba yanaviashiria vya rushwa, udanganyifu na ubahirifupi.	416.89	590.44	116.74	1,124.07	63
Jumla	560.19	863.85	346.80	1,770.84	100
Asilimia (%)	32	49	20	100	

**Jambo la 1: Uwezekano wa Serikali Kupoteza Mapato ya TZS 265.85 Bilioni**

Kutokana na udhaifu katika mifumo ya ukusanyaji wa mapato, kuna uwezekano mkubwa wa Serikali kupoteza TZS 265.85 bilioni kutokana na vitendo vya rushwa, udanganyifu na ubahirifupi kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 5. Katika Serikali Kuu, kumekuwa na ongezeko la upotevu wa mapato kutoka TZS 7.70 bilioni kwa mwaka 2018/19 mpaka TZS 38.70 bilioni kwa mwaka 2019/20 ikiwa ni ongezeko la TZS 31.00 bilioni.

**Jedwali Na. 5: Mchanganuo wa kiasi ambacho kinaonesha viashiria vya rushwa, udanganyifu na ubahirifupi katika ukusanyaji wa mapato katika Serikali Kuu, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mashirika ya Umma.**

Mwaka	Serikali Kuu	Serikali Za Mitaa	Mashirika ya Umma	Jumla
<b>TZS Bilioni</b>				
2018/19	7.70	44.03	-	51.73
2019/20	38.70	191.20	35.96	265.85
Ongezeko la upotevu	31.00	147.17	35.96	214.12
Asilimia	403	334	100	414

### Serikali Kuu:

Katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali Kuu, CAG alibaini mapungufu yafuatayo:

- Kupotea kwa kodi ya TZS 12.14 bilioni ya mafuta lita 16.55 milioni yaliyoingizwa nchini kama mafuta ambayo yalikuwa yanaenda nchi jirani lakini hayakutoka nje ya nchi.
- Kutokusanya kwa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) ya TZS 8.90 bilioni kutokana na wafanyabiashara kushusha thamani ya mauzo katika ripoti zao za mwezi.
- Upotevu wa makusanyo yenye thamani ya TZS 1.24 bilioni yaliyokusanya nje ya mfumo wa malipo ya Serikali GePG na ambayo hayakupelekwa benki.




### Serikali za Mitaa:

Baadhi ya mapungufu yaliyopelekea upotevu wa TZS 191.20 bilioni, katika ukusanyaji wa mapato ya ndani katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa ni kama yafuatayo:

- Kutokana na Ukaguzi maalumu katika ukusanyaji wa mapato ya ndani ya MSM 43 kwa kipindi cha miaka mitatu (2017/18 - 2019/20), CAG alibaini kutokusanya kwa TZS 60.81 bilioni ambazo ni mapato ya ndani yaliyopaswa kukusanya.
- Katika ukaguzi wa mwaka 2019/20, CAG ameonesha kuongezeka kwa kutokusanya kwa mapato ya ndani kwa kipindi cha mwaka 2016/17 hadi 2019/20 kama ifuatavyo:

## Mapato ambayo hayakukusanywa



- c. Mapitio ya mfumo wa mapato (LGRCIS) katika MSM 67 yalionesha kulikuwa na TZS 35.99 bilioni ambazo ni miamala iliyokuwa haijawasilishwa na wakusanya mapato kutoka kwenye vyanzo mbalimbali. Baadhi ya Halmashauri zilizokuwa na hoja hii ni kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Na. 6.

**Jedwali Na. 6: Miamala ambayo ilikuwa haijawasilishwa na wakusanya mapato kutoka kwenye vyanzo mbalimbali**

Na	Halmashauri	Mapato ya Ndani (TZS Milioni)	Kiasi Kinachodaiwa (TZS Milioni)	Asilimia
1	H/W Tandahimba	4,374.53	24.85	0.57
2	H/M Songea	3,429.50	26.62	0.78
3	H/W Mkinga	1,096.09	57.12	5.21
4	H/W Gairo	640.25	89.61	13.99
5	H/M Ilala	58,649.46	117.46	0.20
6	H/W Songea	1,060.52	174.62	16.46
7	H/W Nanyumbu	2,007.33	250.18	12.46
8	H/Mji Ifakara	1,963.59	522.22	26.59
9	H/W Pangani	1,263.62	24.83	1.96
10	H/Mji Handeni	1,225.66	67.07	5.47

- d. Katika ukaguzi maalumu wa mfumo wa ukusanyaji mapato kwa kipindi cha miaka mitatu (2017/18 - 2019/20), CAG alibaini mawakala wa kukusanya mapato katika MSM 59 hawakupeleka benki makusanyo ya TZS 23.88 bilioni yaliyokusanywa kuititia mashine za POS. Hii ilitokana na MSM kuwa na udhaifu katika usimamizi wa ndani wa mfumo huo wa ukusanyaji mapato. Baadhi ya MSM zilizokuwa na kasoro hii ni kama zifuatazo:

**Baadhi ya Halmashauri ambazo mawakala wa kukusanya mapato hawakupeleka benki makusanyo:**

NA	HALMASHAURI	Mapato ya Ndani	Kiasi ambacho Hakikupelekwa Benki	Asilimia
(TZS Millioni)				
1	H/W Kilosa	3,809.47	713.7	18.73
2	H/W Sumbawanga	2,426.85	418.11	17.22
3	H/Mji Kahama	8,122.80	78.76	0.96
4	H/M Tabora	3,166.76	34.79	1.09
5	H/M Ilala	58,649.46	552.46	0.94
6	H/W Songea	1,060.52	1,011	95.33
7	H/W Njombe	5,995.09	32.86	0.54
8	H/W Mkinga	1,096.09	21.46	1.96

**Mashirika ya Umma:**

Katika ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Mashirika ya Umma, baadhi ya mapungufu yaliyopelekea upotevu wa TZS 35.96 bilioni ni kama yafuatayo:

- a. Upotevu wa TZS 20.17 bilioni kutokana na kufutwa kwa madeni ya wakopaji pasipo kuwa na idhini ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Wizara ya Fedha na Mipango ambayo ni kinyume na kanuni ya 22(3) ya Kanuni ya Sheria ya Fedha za Umma ya Mwaka 2001(kama ilivyorekebishwa) kama inavyonekana katika Jedwali Na. 7.

**Jedwali Na. 7: Mashirika Yaliyofuta Madeni Pasipokuwa na Idhini ya Wizara ya Fedha na Mipango na Ofisi ya Msajili wa Hazina.**

Taasisi	Disemba 2018	Disemba 2019
	TZS Bilioni	
Benki ya Maendeleo TIB	0.69	9.02
TPB Benki	12.53	11.15
<b>JUMLA</b>	<b>13.22</b>	<b>12.17</b>

- b. Upotevu wa makusanyo yenyeye thamani ya TZS 7.23 bilioni yaliyokusanywa nje ya mfumo wa malipo ya Serikali GePG na hayakupelekwa benki.
- c. Upotevu wa mapato yenyeye thamani ya TZS 2.25 bilioni kutokana na msamaha usiostahili uliotolewa kwa Kampuni ya Saruji ya Mbeya.

## Athari

Fedha zilizokusanywa na kutopelekwa benki, ni dhahiri kuwa fedha hizi zimeibwa na wakusanyaji wa mapato hayo. Vilevile, kuna uwezekano wa Serikali kupoteza mapato ya TZS 265.85 bilioni kutokana na vitendo vinavyoashiria rushwa, udanganyifu na ubahirifupi. Upotevu huu unaweza kuisababishia Serikali kushindwa kufikia lengo la makusanyo kama ilivyoidhinishwa katika bajeti ya Taifa. Kiasi hiki kingeweza kukamilisha miradi ya maendeleo ambayo haikupokea fedha kwa mwaka 2019/20 na kuwakosesha wananchi fursa ya kupata huduma za kijamii.

## Ushauri:

Ili kutatua changamoto zilizobainishwa, WAJIBU inashauri yafuatayo:

- a) Mamlaka ya Serikali Mtando (eGA) kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango ifanye mapitio ya mifumo yote ya TEHAMA inayohusika katika usimamizi wa ukusanyaji wa mapato ya umma ili:
  - i. Kuongeza udhibiti wa matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali (mfano, LGRCIS na GePG) na
  - ii. Kuhakikisha kunakuwa na ufanisi wa uendeshaji wa mifumo ya TEHAMA Serikalini ili kuondoa vitendo vya rushwa, udanganyifu na ubahirifupi.
- b) Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ifanye uchunguzi na kuwachukulia hatua wale wote watakaobainika kwa namna moja au nyininge wamejihusisha na vitendo vya rushwa, udanganyifu na ubahirifupi vilivyopeleke upotevu wa mapato ya ndani.
- c) OR-TAMISEMI kupitia kitengo cha ufuatiliaji wa fedha katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa (IFTU) kifanye ukaguzi maalumu katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea ambapo kiasi cha asilimia 95.33 hakikupelekwa benki.



## Jambo la 2: Matumizi Yasiyo na Tija TZS 380.92 Bilioni katika Matumizi ya Kawaida

CAG ameonesha, kuwepo kwa viashiria vya rushwa, udanganyifu na ubadhirifu katika matumizi ya TZS 380.92 bilioni kwa mwaka 2019/20 yaliyotokana na udhaifu wa mifumo ya ndani katika usimamizi wa matumizi ya kawaida. Thamani ya kiasi cha TZS 380.92 bilioni ni ongezeko la asilimia 2,511 ikilinganishwa na TZS 14.59 bilioni ya mwaka 2018/19 kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 8.

**Jedwali Na. 8: Mchanganuo wa kiasi ambacho kina viashiria vya rushwa, ubadhirifu na udanganyifu katika Matumizi ya kawaida katika Serikali Kuu, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mashirika ya Umma.**

	Serikali Kuu	Serikali za Mitaa	Mashirika ya Umma	Jumla
<b>TZS Bilioni</b>				
2018/19	0.20	0.64	13.75	14.59
2019/20	104.60	82.21	194.11	380.92
Ongezeko	104.40	81.57	180.36	366.33
Asilimia	52,200	12,745	1,312	2,511

**MUHIMU:** Ongezeko la asilimia 52,200 ya matumizi ya kawaida yenye viashiria vya udanganyifu na ubadhirifu kwa mwaka 2018/19 kwa Serikali kuu ni kiasi kikubwa na kinaonesha ni namna gani mifumo ya ndani ya usimamizi wa matumizi ya kawaida imeshindwa kudhibiti udanganyifu na ubadhirifu katika matumizi hayo. Vivyohivyo, katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa kumekuwa na ongezeko la asilimia 12,745 ya matumizi yenye viashiria vya udanganyifu na ubadhirifu katika matumizi ya kawaida.

### Serikali Kuu

Baadhi ya maeneo yaliyokuwa na viashiria vya rushwa, udanganyifu na ubadhirifu katika Serikali Kuu kwenye matumizi ya kawaida, ni kama ifuatavyo:

- Miradi minne ya sekta ya uchukuzi ilikuwa na tozo ya riba kiasi cha TZS 8.18 bilioni kama adhabu ya kuchelewesha kulipa madai ya makandarasi (IPCs). Uchambuzi unaonesha kuwa, sekta ya uchukuzi inaongoza kuchelewesha malipo ya makandarasi ambapo TZS 3.47 bilioni ilihuisha Programu ya Kusaidia Sekta ya Usafirishaji (TSSP), Mradi wa Maendeleo ya Reli Tanzania (TIRDP) TZS 2.20 bilioni, Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Kimataifa Arusha-Taveta/Holilii/Voi TZS 1.85 bilioni na Mradi wa Uboreshaji Usafiri wa Mjini Dar es Salaam (DUTP) TZS 0.67 bilioni.
- Udhaifu katika usimamizi wa matumizi uliosababisha watumishi kutorudisha masurufu ya TZS 6.80 bilioni na watumishi hao kutoanza kukatwa mishahara yao kama sheria ya fedha inavyoelekeza.

- c) Katika taasisi 12, CAG alishindwa kuhakiki matumizi ya TZS 5.74 bilioni yenye viambatisho pungufu hivyo kutia shaka uhalali wa matumizi hayo.
- d) Matumizi ya TZS 34.99 bilioni katika Mfuko wa Maendeleo ya Utalii yanetumika pasipo kuwa na nyaraka zilizoidhinishwa.



### Mamlaka ya Serikali za Mitaa

Baadhi ya maeneo yaliyokuwa na viashiria vya rushwa, udanganyifu na ubahirifupi katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa, ni kama yafuatayo:

- a) MSM 86 zilifanya matumizi ya TZS 9.83 bilioni katika akaunti ya amana pasipo kufuata taratibu za uendeshaji wa akaunti hiyo. Kasoro hizo ni pamoja na:

Na.	Kasoro	Idadi ya MSM	Kiasi TZS Bilioni
1.	Malipo ambayo hayakuidhinishwa	30	2.45
2.	Kulipa miradi fedha zaidi ya kiasi kilichowekwa katika akaunti ya amana	28	4.60
3.	Mikopo isiyorejeshwa kwenye akaunti ya amana	28	2.78
<b>JUMLA</b>		<b>86</b>	<b>9.83</b>

- b) MSM zililipa TZS 9.88 bilioni kama gharama ya kodi ya ongezeko katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambayo ilikuwa imesamehewa kodi ya ongezeko la thamani. Miradi iliyolipiwa kodi hiyo ingali imesamehewa ni ile inayotekelizwa na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, Wizara ya Fedha na Mipango, TANROADS, MWAUWASA na AUWASA.
- c) MSM 130 hazikukusanya TZS 27.79 bilioni ambayo ni marejesho ya mikopo iliyotolewa kwa vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenyeulemavu. Katika ukaguzi wake, CAG alibaini MSM 130 zilitoa jumla ya TZS 42.94 bilioni na kukusanya marejesho ya TZS 1770 bilioni sawa na asilimia 41. Hata hivyo, mbali na Serikali kurekebisha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa ya 1982 ili kuboresha usimamizi na uendeshaji wa mfuko wa uwezeshaji wa vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenyeulemavu, bado urejeshwaji wa mikopo hiyo hauridhishi. Ripoti ya CAG imeonesha kuongezeka kwa mikopo ambayo haijarejeshwa kwa kipindi cha miaka mitatu kama inavyooneshwa kwenye jedwali. Na. 9.

#### Jedwali Na.9: Asilimia ya mikopo ambayo haikurejeshwa kwa mwaka 2017/18 - 2019/20

Mwaka	Idadi ya Halmashauri	Fedha ambazo hazijarejeshwa (TZS Bilioni)	Fedha ambazo hazijarejeshwa (%)
2019/20	130	27.79	65
2018/19	111	13.79	59
2017/18	90	10.04	59

#### Mashirika ya Umma:

Baadhi ya maeneo yaliyokuwa na viashiria vya rushwa, udanganyifu na ubadhirifu kwenye matumizi ya kawaida katika Mashirika ya Umma, ni kama yafuatayo:

- a) Uwezekano wa Shirika la Nyumba Kulipa riba kubwa kutokana na kukopa kuitia huduma ya mikopo ya muda mfupi “overdraft” kiasi cha TZS 4.70 bilioni bila kuwa na mkataba na Benki ya NMB.
- b) Upotevu wa TZS 3.93 bilioni kutokana na miamala ya udanganyifu katika bandari ya Kigoma na Mwanza uliosababishwa na udhaifu katika usimamizi wa malipo.
- c) Malipo ya TZS 4.95 bilioni yaliyolipa bila ya kuwa na nyaraka kamili hivyo kuwa na viashiria vya rushwa, udanganyifu na ubadhirifu.

#### Athari:

Udhaifu katika usimamizi wa gharama ya matumizi ya kawaida uliosababishwa na uwepo wa viashiria vya rushwa, udanganyifu na ubadhirifu umepelekea kuwepo na upotevu wa fedha au matumizi yasiyo na tija, hivyo kutokuwepo na thamani ya fedha katika malipo ya TZS 380.92 bilioni. Hii imesababisha Serikali kupoteza fedha ambazo zingeweza kutumika katika kuajiri watumishi 119,753 kwenye MSM 123 zilizokuwa na upungufu wa watumishi kwa mwaka 2019/20.

# TZs 380.92 bilioni

Kiasi cha fedha ambazo Serikali imepoteza kwa njia ya rushwa, udanganyifu na ubahiriflu au matumizi yasiyo na tija.

## Ushauri:

WAJIBU inashauri kuwa Wizara ya Fedha na Mipango itoe fedha za utekelezaji wa miradi kwa wakati ili kupunguza ongezeko la tozo za riba kutoka kwa makandarasi. Aidha, TAKUKURU ifanye uchunguzi katika taasisi zilizoripotiva kusababisha upotevu wa fedha za umma au kufanya matumizi yasiyo na tija ili kuwafikisha mahakamani wahuksika wote watakaokuwa wamehusika katika vitendo vya rushwa, udanganyifu na ubahiriflu.

## Jambo la 3: Matumizi ya TZS 1,124.07 bilioni katika Ununuzi wa Umma na Usimamizi wa Mikataba yana viashiria vya Rushwa, Ubahiriflu na Udanganyifu

Katika ununuzi wa umma na usimamizi wa mikataba kuna hatari ya TZS 1,124.07 bilioni kuwa zimetumika bila kuleta tija kutokana na kuwa na viashiria vya rushwa, udanganyifu na ubahiriflu. Kiasi hiki kimeongezeka kwa TZS 957.87 bilioni sawa na asilimia 576 kutoka TZS 166.20 bilioni ya mwaka 2018/19.

Kumekuwa na kiasi kikubwa cha matumizi katika ununuzi wa umma na usimamizi wa mikataba ambayo yana viashiria vya rushwa, udanganyifu na ubahiriflu hususani kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kiasi cha TZS 590.44 bilioni, ikifuaatiwa na Serikali Kuu TZS 416.89 bilioni na Mashirika ya Umma TZS 116.74 bilioni kama inavyoonekana katika Jedwali Na . 10.

## Jedwali Na. 10: Mchanganuo wa kiasi ambacho kinaviashiria vya rushwa, ubahiriflu na udanganyifu katika Ununuzi wa Umma na Usimamizi wa Mikataba katika Serikali Kuu, Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Mashirika ya Umma

	Serikali Kuu	Serikali za Mitaa	Mashirika ya Umma	Jumla
TZS Bilioni				
2018/19	26.40	59.26	80.54	166.20
2019/20	416.89	590.44	116.74	1,124.07
Ongezeko	390.49	531.18	36.20	957.87
Asilimia	1,479	896	45	576

## Serikali Kuu:

Baadhi ya kasoro zilizopelekea kuwepo kwa viashiria vya rushwa, udanganyifu na ubahiriflu katika Ununuzi wa Umma na Usimamizi wa Mikataba katika Serikali kuu ni pamoja na:

katika ununuzi wa umma na usimamizi wa mikataba katika Serikali Kuu ni pamoja na:

- Kuwepo kwa malipo yenye shaka katika uwekezaji wa Mradi wa Mfumo Salama wa Mawasiliano (Independent Mobile Secured Network) TZS 129.56 bilioni,
- Kutopatikana kwa thamani ya fedha katika matumizi ya TZS 69.82 bilioni kutokana na kuchelewa kukamilika kwa ujenzi wa miradi 21 ya ujenzi na kuchelewa kupokea bidhaa na huduma, na
- Mapungufu katika usimamizi wa ujenzi wa ofisi za mahakama 42 zenyet thamani ya TZS 40.95 bilioni.

#### Mamlaka ya Serikali za Mitaa:

Baadhi ya kasoro zilizopelekea kuwepo kwa viashiria vya rushwa, udanganyifu na ubahirifu katika ununuzi wa umma na usimamizi wa mikataba katika MSM ni pamoja na:

- Kuwepo hatari ya ongezeko la gharama za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kutokana na kuongezeka kwa muda wa makandarasi katika maeneo ya miradi pamoja na kupanda kwa bei za bidhaa katika MSM 101 ambazo ziliwa na miradi yenye thamani ya TZS 184.01 bilioni iliyochelwa kukamilika. MSM zenyet miradi ya maendeleo ambayo hajakamilika zimeongezeka kutoka 26 mwaka 2016/17 hadi 101 mwaka 2019/20 na thamani ya miradi ambayo hajakamilika imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka kutoka TZS 3.19 bilioni mwaka 2016/17 hadi TZS 184.01 bilioni mwaka 2019/20. Kuendelea kuongezeka kwa miradi ambayo hajakamilika inasababishwa na Serikali kuwa na idadi kubwa ya miradi inayopangwa kutekelezwa kuliko uwezo wa kifedha katika mwaka husika. Jedwali Na. 11 linaonesha ongezeko la miradi isiyokamilika kwenye MSM.

**Jedwali Na. 11. Ongezeko la miradi isiyokamilika kwenye MSM kwa kipindi cha miaka minne (2016/17 – 2019/20)**

Mwaka	2016/17	2017/18	2018/19	2019/20	TZS Bilioni
					TZS Bilioni
Thamani ya Miradi ambayo hajakamilika	3.19	52.43	77.51	184.01	
Idadi ya MSM	26	47	81	101	

**Baadhi ya MSM zilizokuwa na miradi ambayo haikukamilika ni pamoja na:**

Na	Halmashauri	Mradi	Gharama (TZS Milioni)
1	H/W Bukoba	Ujenzi wa ukumbi wa bwalo la chakula na maktaba katika Shule ya Sekondari Kagemo	170.00
2	H/W Nkasi	Ujenzi wa kituo cha afya cha Ninde	200.00
		Ujenzi wa hospitali ya Wilaya	300.00
3	H/W Sumbawanga	Ujenzi wa hospitali ya Wilaya	1,800.00
4	H/W Kilosa	Visima vinne katika Kijiji cha Ng'ole, Changalawe, Chabi na Mgogozi	28.00
5	H/W Njombe	Ujenzi wa mradi wa maji katika Kijiji cha Matembwe/Lyembela	996.94
		Ujenzi wa pampu ya maji Kijiji cha Lupembe	848.37
		Ujenzi wa mradi wa maji Kijiji cha Kidgembye	1,354.31

- Miradi yenye thamani ya TZS 51.27 bilioni ilikuwa inatekelezwa pasipo kuwa na hati halali za dhamana ya utendaji. Kutokuwepo kwa hati halali za dhamana ya utendaji kunaweza kuliingizia taifa hasara kwani endapo mkandarasi atashindwa kutekeleza mradi kwa ufanisi, Serikali haitakuwa na uwezo wa kupata fidia ya hasara

iliyojitekeza kutoka kwa mkandarasi.

- c) Kuwepo kwa viashiria vya rushwa, udanganyifu na ubahirifupi kutokana na kushindwa kuwasilisha kwa mkaguzi wa hesabu nyaraka za zabuni na ripoti za tathmini za zabuni za mikataba yenye thamani ya TZS 39.50 bilioni iliyoingiwa baina ya MSM na wataalamu washauri 12.

### **Mashirika ya Umma:**

Baadhi ya kasoro zilizopelekea kuwepo kwa viashiria vya rushwa, udanganyifu na ubahirifupi katika ununuzi wa umma na usimamizi wa mikataba katika Mashirika ya Umma ni pamoja na:

- a) Zabuni zilitolewa juu ya kiwango cha daraja la makandarasi. CAG alibaini miradi 3 iliyoingiwa na Mamlaka ya Bandari Tanzania yenye thamani ya TZS 25.90 bilioni ilitekelezwa na makandarasi walio chini ya kikomo cha daraja kilichowekwa na Bodi ya Usajili wa Makandarasi hivyo kusababisha miradi kuchelewa kukamilika,
- b) Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) ilifanya malipo ya Dola za Marekani 29.60 milioni (sawa na TZS 60 bilioni) bila kukata kodi ya zuio,
- c) Uwezekano wa kupotea kwa kiasi cha TZS 18.81 bilioni kama gharama za awali zilizotumika katika kutekeleza miradi 6 ya mamlaka za maji katika Mikoa ya Dar es Salaam, Kilimanjaro na Arusha. Miradi hii imetelekezwa kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo.

### **Athari**

Udhaifu katika ununuzi wa umma na usimamizi wa mikataba uliosababishwa na uwepo wa viashiria vya rushwa, udanganyifu na ubahirifupi umepelekea matumizi yasiyo na tija ya TZS 1,124.07 bilioni na kusababisha athari zifuatazo;

- a) Kiasi cha TZS 1,124.07 bilioni cha matumizi yasiyo na tija kingewezesha Serikali kutoa kiasi chote cha bajeti ya miradi ya maendeleo kwa mwaka 2019/20 ambapo MSM 152 hazikupokea TZS 410.48 bilioni sawa na asilimia 46 ya bajeti iliyoingiwa.
- b) Kiasi ambacho kimepotea kingeweza kutumika katika kuwapunguzia wananchi adha ya upatikanaji wa huduma za maji, afya na elimu. Mfano, Kijiji cha Masanula kilichopopo kata ya Usule Wilayani Shinyanga hakina zahanati tangu kilipoanzishwa mwaka 1969.

### **Ushauri**

Ili kuondoa viashiria vya rushwa, udanganyifu na ubahirifupi katika ununuzi wa umma na usimamizi wa mikataba, WAJIBU inashauri yafuatayo:

- a) TAKUKURU iweke mkazo katika kutambua viashiria vya rushwa, udanganyifu na ubahirifupi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hii ifanyike kwa kuboresha utendaji wa Idara ya Ufuatiliaji wa Matumizi ya Serikali (PETS) kwa kuwaongezea idadi ya watumishi wa Idara hiyo katika ngazi ya Wilaya na kuwapatia vitendea kazi.
- b) Kuwepo na ushirikiano wa utendaji kazi wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi na Ofisi za Usimamiaji wa Sheria hapa nchini kulingana na matakwa ya utekezaji wa matakwa ya Kifungu cha 27 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma 2008 (kama iliyyorekebishesha).

- c) Ili kuboresha ushirikiano uliopo kati ya Ofisi ya TAKUKURU, AZAKI, Vyombo vya Habari na Wananchi, TAKUKURU iongeze kutoa mrejesho kwa wadau ikiwa ni pamoja na kuiwasilisha ripoti ya utendaji wake ya mwaka bungeni ili kuifanya ripoti hiyo kujadiliwa na kuwa wazi kwa umma.
- d) TRA ishirikiane na Kampuni ya Huduma za Meli ili kupata kodi ya zuij ambayo haikutozwa kutoka kwenye malipo ya Dola za Marekani 29.60 milioni.

# HITIMISHO

Ripoti hii imeonesha kuna udhaifu mkubwa katika utendaji wa mifumo ya usimamizi wa fedha za umma hivyo, kuathiri utekelezaji wa sera na mipango mikakati ya nchi. Maeneo yaliyoathirika ni pamoja na; utoaji wa vitambulisho nya taifa, miundombinu ya masoko ya chakula, mifumo ya TEHAMA, ukusanyaji wa Kodi ya “Uhamishaji Gharama” ya mauziano (Transfer Pricing), mradi wa uzalishaji wa sukari Mbigiri na miradi iliyotekelawa kwa utaratibu wa “Force Account” katika sekta ya elimu.

Aidha, uchambuzi unaonesha viashiria nya rushwa, udanganyifu na ubahirifupi vimeongezeka ukilinganisha na mwaka 2018/19. Ongezeko hili, limetokea zaidi katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa hususani katika eneo la ununuza wa umma na usimamizi wa mikataba ambapo kiasi kilichokuwa na viashiria nya rushwa, udanganyifu na ubahirifupi ni TZS 590.44 bilioni. Hii inatia shaka endapo Serikali imepata tija katika ununuza wa umma na usimamizi wa mikataba.

**WAJIBU** inatoa wito kwa wadau wa uwajibikaji kutumia ripoti hii kama chanzo cha taarifa katika ufuatiliaji wa mapato na matumizi ya rasilimali za umma. Ufuatiliaji huo unaweza kutumia mbinu mbalimbali kama vile kuhoji kupitia vyombo nya habari, mikutano/midahalo na watendaji wa Serikali, kutumia nyenzo ya uwajibikaji jamii (SAM) au ufuatiliaji wa matumizi ya rasilimali za umma (PETS), kutoa taarifa na kushirikiana na vyombo nya dola kama TAKUKURU katika kupambana na vitendo nya rushwa, udanganyifu na ubahirifupi.

Vilevile, unaweza kupakua ripoti hii ya uwajibikaji kupitia tovuti ya WAJIBU [www.wajibu.or.tz](http://www.wajibu.or.tz) au kutufuatilia katika mitando ya kijamii; Instagram, twitter na facebook [@wajibu\\_institute](https://www.facebook.com/wajibu_institute).

**MUHIMU:** Ili kupata taarifa zaidi kuhusu ripoti za CAG za mwaka 2019/20, tembelea tovuti ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT) [www.nao.go.tz](http://www.nao.go.tz)







Mawasiliano:

**WAJIBU - INSTITUTE OF PUBLIC ACCOUNTABILITY**

S.L.P13486,  
Rose Garden Road, Ndovu Street, House No.10,  
Dar es Salaam  
Email: wajibu.institute@gmail.com



Wajibu\_Institute



Wajibu\_Institute



WAJIBU\_Institute of Public Accountability



WAJIBU\_Institute of Public Accountability